TANGAZO LA SERIKALI Na. 108 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA DODOMA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Dodoma ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango miji na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama.

*Tangazo la Serikali Na. 108 (linaendelea)*

______

JEDWALI

______

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 468190.67MS, 9576276.56KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa KS60$^0$42'41.99''MS kwa umbali wa kilomita 1.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 469807.12MS, 9575580.17KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS29$^0$37'49.96''MS kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 468670.23 MS, 9573581.13; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ58$^0$06'20.22''MG kwa umbali wa kilomita 1.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 467137.28MS, 9574535.72KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ31$^0$09'59.72''MG kwa umbali wa kilomita 2 hadi ulipoanzia.''

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*